

Sababu za Kudondoshwa kwa Fonimu za Likwidi katika Maneno Teule.

Evans Kiplimo Cheruiyot
Kenyatta University, Kenya.

Email: cheruiyotevanskiplimo@gmail.com

IKISIRI

Utafiti huu umelenga kuchunguza sababu za kudondoshwa kwa fonimu za likwidi katika maneno teule. Uchanganuzi huu umeongozwa na nadharia ya fonolojia zalishi. Utafiti huu umetegemea data ya maktabani iliyokusanywa kupitia kwa mbinu za kusoma na kudondoa. Ili kushughulikia tatizo la utafiti kikamilifu, utafiti huu ulitegemea aina tatu ya data. Kwanza, data ya maumbo yaliyopangwa upya kwa matumizi ya mbinu linganishi na uundaji ndani. Pili, data kutoka kwa *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Data hii iliteuliwa kimaksudi kwa sababu inaweza kutosheleza katika kushughulikia tatizo la utafiti. Data ya makala hii imechanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo. Makala hii ilibainisha kuwa ni vigumu kutenganisha vichocheo na sababu kamili za mabadiliko ya lugha. Pili, athari za mabadiliko ya lugha zinaweza kuingizwa kama maelezo ya sababu za mabadiliko ya lugha. Tatu, ilikuwa vigumu kubainisha mipaka baina ya sababu za kiisimu na kiisimu-jamii. Utafiti huu ulihitimisha kuwa kuwa mabadiliko mengine kama vile uchopekaji hutokea katika kiwango cha mofolojia ili kurekebisha makosa ya kimuundo katika lugha yanayosababishwa na badiliko la kwanza. Kando na haya, makala hii ilionyesha kuwa sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi haina tija katika Kiswahili cha sasa. Utafiti huu unapendekeza kuwa Kuzuia uhomonimia na kuwepo kwa masalio ya kiisimu ni baadhi ya sababu zilizotolewa kueleza uzuiaji wa sheria.

Maneno muhimu: Urahisishaji, utashi wa wazungumzaji, tija, sheria ya uziada na uzuiaji wa sheria.


How to cite this article in APA.

Cheruiyot, E. K. (2022). Sababu za Kudondoshwa kwa Fonimu za Likwidi katika Maneno Teule. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 4(1), 348-355. DOI: <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.299>

UTANGULIZI

Mabadiliko ya lugha ni ugeukaji wa muundo wa kipengele chochote kinachohusiana na lugha. Udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi ni mchakato wa kifonolojia unaoathiri utokeaji wa fonimu za likwidi katika maneno teule ya Kiswahili. Kiplimo na Mwita (2021) walibaini kuwa badiliko hili liliathiri maneno ya Kiswahili ya asili ya Kibantu yenye mfuatano wa vokali mbili kama vile, *mzee* na *kaa*. Maneno haya yalikuwa na fonimu /r/ au /l/ katikati ya vokali kama sehemu ya kijenzi cha neno kabla ya mabadiliko kutokea.

Visababishi vya mabadiliko ya lugha hurejelea mambo ambayo huleta mabadiliko na mazingira yanayoweza mabadiliko. Tunaweza kueleza sababu za mabadiliko ya kihistoria iwapo tutaelewa kuwa mabadiliko katika mpito wa wakati hutokana na tofauti zilizokuwepo katika maumbo ya awali ya lugha. Aitchison (1991) akimrejelea Saussure (1915), alifaninisha isimu daikronia na isimu sinkronia kwa matumizi ya analojia ya shina la mti kama ifuatavyo:



Asili: www.google.com/search

Kielelezo 1: Analojia ya shina la mti

Mkato-wima huashiria uchunguzi wa lugha kwa wakati maalum ilhali ukato wa kimlalo huashiria ukuaji wa vipengele mbalimbali vya lugha katika kipindi kirefu. Tofauti za kisinkroniki ni kichocheo cha mabadiliko ya kidaikronia (McGregor, 2009). Uchanganuzi wa kidaikronia upo katika msingi wa kulinganisha na kulinganua uchanganuzi wa kisinkroniki wa lugha katika vipindi mbalimbali. Maelezo

haya yanaafikiana na maelezo ya Aitchison (1991) anaposema kuwa, isimu sinkronia ilitangulia isimu daikronia. Uchanganuzi wa kisinkronia wa maumbo yenye upekee fulani kama vile *kaa/kalia* yanaweza kuelezwa kidaikronia.

MAPITIO YA MAANDISHI

Wataalamu mbalimbali wakiwemo Hinnebusch (1973), Schane (1973), Mgullu (1999), Crowley & Bower (2010) na Massamba (2011) wameshughulikia aina anuwai za udondoshaji katika lugha mbalimbali. Kati ya watafiti hawa, Hinnebusch (1973) alipokuwa akitoa mahitimisho kuhusu mabadiliko ya kihistoria katika lugha za pwani ya Kenya, aliorodhesha udondoshaji wa fonimu /l/ katika Kiswahili kama badiliko la kihistoria. Nao Mgullu (1999) na Habwe na Karanja (2004) wametaja na kueleza udondoshaji wa kihistoria wa fonimu /r/ na /l/ katika mazingira ya kuwepo katikati ya vokali mbili kwenye maneno ya Kiswahili. Katika utafiti wa hivi karibuni wa upangaji upya wa leksika za Kibantu, Bostoen & Bastin (2016) walibainisha fonimu /l/ kama sauti bora ya kupangwa upya katika misingi ya mbinu linganishi. Walifikia uamuzi huu baada ya kubainisha fonimu /l/ kama sauti linganifu iliyokuwepo katika lugha teule zikiwemo Kisotho, Isizulu, Kikongo na Simakonde isipokuwa Kiswahili. Nao Kiplimo na Mwita (2021) walitumia nadharia ya fonolojia zalishi pamoja na mbinu za ujenzi upya wa lugha (mbinu linganishi na uundaji ndani) kudhihirisha kuwa fonimu za likwidi zilidondoshwa katika mazingira ya kuwepo katikati ya vokali mbili.

Mbinu linganishi ilionyesha kuwa fonimu za likwidi zipo katika maneno ya lugha teule za Kibantu isipokuwa Kiswahili. Fonimu za likwidi kuwepo kwa lugha teule za Kibantu ni kwa sababu ni sifa iliyokuwepo katika mame lugha. Katika matumizi ya mbinu ya uundaji ndani ilibainika kuwa kuchopekwa kwa fonimu /l/ katika mnyambuliko wa vitenzi teule vya Kiswahili katika kauli ya kutendea ni ruwaza inayoonekana na yenye upekee. Mbinu ya uundaji ndani ilibainisha fonimu /l/ kama umbo lililokuwepo katika

neni asilia kabla ya mabadiliko ya udondoshaji wa kihistoria kutokea. Utafiti huu una umuhimu kwa kuwa ilifidia pengo lililokuwepo katika lugha. Hata hivyo, hawajaeleza sababu zilizochochea udondoshaji wa fonimu za likwidi katika mazingira ya kuwepo katikati ya vokali mbili. Je, ni kwa nini badiliko hili likatokea?

Wanaisimu mbalimbali wakiwemo Aitchison (1991), Campbell (1999), Fromkin, Rodman na Hyams (2002), Fasold & Connor-Linton (2006), Mc Gregor (2009), Crowley & Bower (2010) na Trask (2015) wameegemeza vichocho vya mabadiliko ya lugha kwenye vipengele mbalimbali vikiwemo: maisha ya binadamu, maumbile, mazingira, akili na sosiolojia. Aidha, vichocho hivi ndivyo vimekuwa msingi wa kujadili na kufafanua sababu za kudondoshwa kwa fonimu za likwidi.

MATOKEO YA UTAFITI

Sababu za Udondoshaji wa Fonimu za Likwidi

Badiliko la lugha si jambo la kushangaza kwa sababu lugha ni hai na huhusishwa na binadamu nao binadamu ni viumbe wabunifu hivyo basi, lugha hubadilika kukidhi mahitaji yao. Katika kueleza sababu za kudondoshwa kwa fonimu za likwidi, mhimili wa fonolojia zalishi ambapo sababu hutolewa kueleza kwa nini uchanganuzi uliotolewa ni bora uliongoza hatua hii. Kanuni ya uwekevu ilifaa katika kuonyesha ubora wa sababu iliyotolewa. Haja ya kurahisisha matamshi na utashi wa wazungumzaji ni baadhi ya sababu zilizotolewa ili kueleza mabadiliko ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi. Sababu hizi zinaweza kuainishwa katika makundi mawili yakiwemo: sababu za kiisimu na za kiisimujamii. Sababu hizi zimeelezwa katika sehemu inayofuata:

Sababu za Kiisimu

Sababu za kiisimu ni sababu zitokanazo na muundo wa lugha na akili ya wazungumzaji (isimu-nafsia). Sababu hizi za kiisimu zinahusishwa zaidi na sifa za kifonetiki. Data ifuatayo imetumika kufafanua sababu hii:

(1) a. *jala/ jara > jaa

- b. *julu/ juru > juu
- c. *kala/ kara > kaa
- d. *mgulu/ mguru > mguu
- e. *mzele/ mzere > mzee
- f. *mela/ mera > mea

Kiplimo & Mwita (2021) walionyesha kuwa, maumbo ya awali ya maneno haya yalikuwa na fonimu /r/ au // katikati ya vokali. Neno *au* limetumiwa kwa sababu, kubadilishana nafasi ya utokeaji kwa fonimu za likwidi ni swala la kilahaja katika Kibantu. Alama >, imetumiwa kuonyesha badiliko la kidaikronia. Fonimu za likwidi zilidondoshwa kwa ajili ya kurahisisha matamshi. Maneno ya lugha yanayoelekea kubadilika huonyesha dalili za aina fulani ikiwemo urahisishaji. Miundo changamani ya lugha hubadilika taratibu na kuwa miundo sahili. Kueleza dhana ya urahisishaji kikamilifu katika lugha ni vigumu kwa sababu kile kilicho changamani kwa wazungumzaji fulani si tatizo kwa wazungumzaji wengine (Crowley & Bower, 2010). Hebu tuchunguze maumbo ya awali ya maneno *mguu*, *mzee* na *kaa*:

(2)	Neno linalotumika	Neno asili
	Mguu	mgulu
	Mzee	mguru
	Kaa	mzele
		mzere
		kala
		kara

Fonimu /r/ au // zilikuwepo kama sehemu ya kijenzi cha maneno teule kama ilivyo kwenye mfano wa (2). Fonimu /r/ na // ni sauti za kundi asilia kwa sababu zina uhusiano wa karibu katika utamkaji wao. Hebu tuchunguze sifa bainifu za fonimu /r/ na // kwa mujibu wa Mgullu (1999):

[l]	[r]
<ul style="list-style-type: none"> + konso + kitambaza + ufizi - unazali + ghuna 	<ul style="list-style-type: none"> + konso -kitambaza + ufizi - unazali + ghuna

Tofauti baina ya /l/ na /r/ inatokana na sifa ya [+tamba] na [-tamba]. Katika mfano wa (2), fonimu za likwidi zilizo na ukuruba kimatamshi hudondoshwa kwa ajili ya kurahisisha matamshi. Hivyo, maumbotokeo yakawa ni:

- (3)
- a. Mguru > mguu
 - b. Mzere > mzee
 - c. Kara > kaa

Udhaifu wa binadamu kutamka maneno yaliyo na fonimu zilizo na ukuruba katika utamkaji wao hupelekea fonimu hizo kudondoshwa (Fromkin na wenzake., 2002). Hata hivyo, fonimu zinapodondoshwa kwa ajili ya urahisishaji lugha hupata maumbo changamano ya kifonetiki, miundo changamano ya silabi na kadhalika.

Kimsingi, maneno hutamkwa katika utaratibu wa kufuata silabi. Neno lenye silabi mbili huhitaji nguvu zaidi kutamka kuliko neno lenye silabi moja. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo:


- (4)
- a. *Jala/ jara
 - b. *Julu/ juru
 - c. *Mela/ mera

Maneno *jala/jara na *julu/juru yana silabi mbili hivyo hutamkwa kwa mapigo mawili ya silabi. Ili kurahisisha matamshi na kupunguza nguvu inayohitajika kutamka neno, fonimu za likwidi zilidondoshwa kama ifuatavyo:

- (5)
- a. *Jala/ jara > jaa
 - b. *Julu/ juru > juu
 - c. *Mela/ mera > mea

Kwenye mifano ya 5) a na b, idadi ya silabi imepungua kwa moja. Hata hivyo, si kila wakati fonimu za likwidi

zinapodondoshwa idadi ya silabi hupungua. Katika mfano wa 5)c, sehemu ya mwanzo wa silabi ya pili imetoweka kwa sababu ya kudondoshwa. Sauti zinapodondoshwa maneno hufanywa kuwa mafupi hivyo, nguvu kidogo huhitajika kuyatamka (Crowley & Bower, 2010). Kwa mfano, silabi \$la\$ huhitaji nguvu zaidi kutamka kuliko silabi \$a\$.



Silabi \$la\$ imejengeka kwa sehemu ya mwanzo na kilele ilhali silabi \$a\$ imejengeka kwa sehemu ya kilele pekee. Kama ilivyo katika mfanyiko wa usimilisho, udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi unapotokea, nguvu inayohitajika kutamka neno hupungua. Kanuni ya uwekevu inasisitiza kuwa, ala za matamshi huleta sauti pamoja kwa lengo la kupunguza nguvu na wakati unaohitajika kutamka sauti fulani (Celce-Murcia na wenzake., 2010). Namna moja ya kuleta sauti pamoja ni kupitia kwa mfanyiko wa udondoshaji.

Sababu za Kiisimujamii

Sababu za kiisimujamii hutokana na matumizi ya lugha katika jamii. Hizi ni sababu zisizohusishwa moja kwa moja na mfumo wa lugha. Fonimu za likwidi zilidondoshwa kwa sababu ya matamshi ya wazungumzaji. Kama ilivyo mitindo mipya ya mavazi na magari, mitindo mipya ya wazungumzaji wa lugha haiwezi kutabirika. Data ifuatayo imetumika katika kufafanua sababu za kiisimujamii:

- (6)
- a. Ukengele - ukengee
 - b. Tambara - tambaa
 - c. Mng'aro - mng'ao

d. Mkulu- mkuu

Data hii ni kwa mujibu wa BAKITA (2015: 1079, 980, 678, 662) na inaonyesha mtindo mbadala wa kutamka neno. Kando na hayo, sehemu ya data ya (1) imetumika katika kufafanua sababu za kiisimujamii kama ifuatavyo:

- (7) a. julu/juru > juu
b. Mzele/ mzere > mzee
c. Kala/ kara > kaa

Kulingana na Kiplimo na Mwita (2021), mbinu za ujenzi upya wa lugha zilionyesha kuwa katika Kiswahili cha zamani maneno teule yalikuwa na fonimu za likwidi katikati ya vokali kama ilivyo kwenye mifano ya (7) hapo juu. Huo ndio mtindo wa kikale. Mtindo huu wa kikale umetumika katika *Utenzi wa Hamziyyah* (2005). Utenzi huu umeandikwa kwa lahaja ya Kingozi ambacho ni Kiswahili cha kale. Utenzi huu umerejelewa ili kudhihirisha kuwa, hifadhi ya maandiko ni mbinu bora inayoweza kutumika kuchunguza mabadiliko ya lugha. Matumizi ya sauti [l] katikati ya vokali ni mojawapo ya miundo ya kisarufi ya Kingozi inayopatikana katika *Utenzi wa Hamziyyah* ubeti wa 241 kama ifuatavyo:

	Kingozi		Kiswahili cha sasa	
(8)	a. Kilumbe	>	kiumbe	
	b. Elupe	>	eupe	
	c. Kulu >		kuu	
	d. Kilungo	>	kiungo	(Mutiso,

2005:35)

Kasida hii ina lugha ya kikale ambayo haipatikani katika Kiswahili cha kisasa. Maneno yenye muundo huu wa kisarufi yametumika katika baadhi ya lahaja za Kiswahili. Kwa mfano:

Kiswahili	Tikuu	Siu	Pate
Jomvu	Mvita		
Kuu	ku(r)u	ku(r)u	ku(r)u
kubwa	kubwa		
Mzee	dee	dee	dee
vyele	zee		

Data hii ni kwa mujibu wa Nurse na Hinnebusch (1993: 710, 712). Maneno haya yanapotumika katika ushairi wa Kiswahili cha kisasa huwa na lengo la kuleta mapigo fulani. Kwa sababu ya ushirikiano wa sababu mbalimbali ikiwemo haja ya kuzua mbinu mpya ya utamkaji, fonimu za likwidi zikadondoshwa katika maneno teule kama ifuatavyo:

- (9) a. Zala/ zara > zaa
b. Mzele/ mzere > mzee
c. Kala/ kara > kaa
d. Julu/ juru > juu

Wanadamu wanapenda kubadili mitindo ya kusema kama wanavyopenda kubadili mitindo ya mavazi na nywele (Kipacha, 2007). Mitindo hii hubadilika kwa namna fiche akilini mwa wazungumzaji ili waweze kuendana na wakati. Mzungumzaji wa lugha huibua mtindo mpya wa usemaji kutokana na msamiati wa kawaida uliopo. Kwa mfano:

- (10) a. Ukengele - ukengee
b. Tambara - tambaa
c. Mng'aro - mng'ao
d. Mkulu- mkuu

Hatuna uhibitaji wowote dhidi ya mitindo mipya kwa sababu imechangiwa na tamaduni zetu. Kadri wazungumzaji wanavyotumia mitindo mipya ndivyo lugha inavyobadilika taratibu. Kwa mfano, utamkaji wa neno *kipengee* badala ya *kipengele*.

Japo utashi wa wazungumzaji umetotwa na wanaisimu kama vile Postal (1968) kama sababu mojawapo ya lugha kubadilika, kuna upungufu wa aina fulani kwa sababu kuna masharti zuizi fiche yanayotawala vipengele vinavyoweza kubadilika katika lugha. Kwa mfano; kwenye maneno *swala*, *swara*, *kalamu* na *lala*, mabadiliko ya udondoshaji wa kihistoria hayajashuhudiwa japo mazingira ya udondoshaji yapo. Hoja hii, imejadiliwa katika kijimada kinachofuata. Utashi wa wazungumzaji au mtindo mpya wa usemaji ni kisababishi tu kinachopelekea kuwepo kwa sababu fiche ya mabadiliko ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi.

Tija ya Sheria ya Udondoshaji wa Fonimu za Likwidi

Tija ni uwezo wa sheria ya kifonolojia kutumika katika mazingira maalumu hata kwenye maneno mapya. Tija ni mojawapo ya sifa zinazobainisha sheria za kifonolojia (Hayes, 2009). Hebu tuchunguze data ifuatayo:

- (11) a. Lala
b. Kelele
c. Karamu
d. Karabati
- (12) a. Kalamu (kifaa cha kuandika) b. Karamu (sherehe)
- (13) a. Kioo na choo b. Kiota na chota

Maneno haya yamepakuliwa kutoka kwa *Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015)* ili kuonyesha tija na kueleza sababu ya uzuiaji wa sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi. Mifano katika (11) yana mazingira ya udondoshaji wa fonimu za likwidi ila sheria hiyo haitumiki. Katika mifano ya (12), sheria ya udondoshaji inapofaulu maneno ambayo yangetarajiwa kuibuka ni *kaamu* na *kaamu*. Hata hivyo, maneno haya hayapo kwa sababu ya uzuiaji wa sheria. Maneno haya hufanana katika maumbo ya kifonetiki na kutofautiana kimaana hivyo kusababisha uhomonimia unaozua utata wa kileksia. Kulingana na Campbell (1999), ili kuepuka uhomonimia mabadiliko ya sauti huzuiliwa katika maumbo fulani. Katika taaluma ya leksikografia, maneno haya yangeingizwa kwenye kamusi ya Kiswahili kama vidahizo tofauti iwapo sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi ingefaulu. Ili kuondoa matatizo haya, sheria hii huzuiliwa kama ilivyo kwenye maumbo yafuatayo ya ukaakaishaji:

- (14) a. Kioo (aina ya glasi yenye uwezo wa kuonyesha picha)
b. Choo (chumba cha kuenda haja)

Neno *kioo* lina mazingira ya ukaakaishaji lakini sheria ya ukaakaishaji haifanyi kazi kwa sababu inapofaulu kutakuwepo na neno moja *choo* likirejelea dhana

mbalimbali. Neno *lala* lina fonimu ya likwidi // katikati ya vokali za chini-kati. Mazingira haya ni bora kwa matumizi ya sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi. Hata hivyo, neno hili halijapitia mabadiliko hayo. Tunaweza kurejelea hili kama salio la badiliko la lugha. Kimsingi, masalio haya ni muhimu kwa sababu yanawapa mwanga wanaisimu kuhusu jinsi lugha ilivyokuwa kabla ya mabadiliko kutokea. Hata hivyo, kuna maneno mengi ya Kiswahili ambayo mazingira ya udondoshaji wa likwidi yapo japo sheria hiyo haifanyi kazi. Sheria ya udondoshaji wa kihistoria inaonekana kutokuwa na tija katika Kiswahili cha sasa. Ikumbukwe kuwa, badiliko hili lilikumba maneno ya asili ya Kibantu.

Matatizo Katika Kueleza Sababu za Mabadiliko ya Lugha

Japo mtafiti amefanikiwa kuchunguza sababu za mabadiliko ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi, alikumbana na changamoto mbalimbali. Kwanza, imekuwa vigumu kutenganisha vichocheo na sababu kamili za mabadiliko ya lugha. Wakati uo huo, kichocheo cha lugha kinachopelekea kubadilika kwa lugha kinaweza kuwa sababu kamili ya lugha kubadilika kwa mwanaisimu mwingine. Kwa mfano, Anttila (1972) anadokeza kuwa urahisishaji si sababu ya mabadiliko ya lugha bali unachochewa na vikwazo vya kiakili vya kutaka kutumia nguvu kidogo (uwekevu).

Isitoshe, imekuwa vigumu kubainisha mipaka baina ya sababu za kiisimujamii na kiisimu za mabadiliko ya lugha. Ugumu huu unatokana na ukweli kwamba, lugha huhusishwa na jamii lugha. Mtafiti hana budi kuchunguza sarufi ya jamii anapoangazia mabadiliko ya lugha. Utashi wa wazungumzaji ni sababu ya kijamii japo masuala ya kiisimu yanayohusishwa na lugha za wazungumzaji wenye asili ya Kibantu yameshirikiana katika kujenga hoja hiyo.

Mwanaisimu anapoeleza sababu za udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi anaweza kuingiza athari za badiliko hili katika lugha na vipengele mbalimbali vya kiarudhi. Kwa mfano, mtafiti alipokuwa akieleza urahisishaji

kama sababu mojawapo ya udondoshaji wa fonimu za likwidi, aliweka wazi kuwa urahishaji unaweza kupelekea kuzuka kwa miundo changamano. Kwa hivyo, mwanaisimu anahitajika kuwa makini ili aweze kubaini mipaka baina ya athari na sababu za mabadiliko ya lugha.

Athari za Udondoshaji wa Kihistoria wa Fonimu za likwidi Katika Mofolojia

Mabadiliko ya kifonolojia ya udondoshaji wa fonimu ya likwidi huleta athari katika kiwango cha mofolojia. Sommerstein (1977) akimnukuu Kiparsky (1974b), anasema kuwa sababu mojawapo kuu ya lugha kubadilika ni haja ya kurahisisha matamshi kama ilivyoelezwa (rejelea Sehemu ya sababu za kiisimu). Sommerstein (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa, badiliko linalotokea kwa kupewa msukumo na sababu nyingine linaweza kuleta athari katika mfumo wa lugha. Kwa mfano:

- (15) a. Kaa – *kaia
b. Toa – *toea
c. Noa – *noea

Maumbo haya yanakiuka sheria ya uziada katika Kiswahili unaoruhusu mfuatano wa vokali tatu katika viini ambavyo si matokeo ya mfanyiko wowote wa kifonolojia. Ukiukaji huu ni athari itokanayo na udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi katika mofolojia. Kulingana na Sommerstein (1977), ili kuleta mfumo unaokubalika, badiliko lingine (uchopekaji) linafuatia ili kurekebisha makosa yaliyosababishwa na badiliko la kwanza katika maneno teule (udondoshaji wa fonimu za likwidi). Kimsingi, maneno kama 'kaa' na 'toa' hayapo katika hali yake asili. Hali hii husababisha alomofu tofauti zenye konsonanti katika kauli hiyo ya kutendea. Alomofu zinaweza kutokea kwa sababu ya mifanyiko ya kifonolojia. Wakati mwingine alomofu hizo hurejelewa kama alomofu za kifonolojia. Kwa hiyo, maumbo hayo huchopekwa fonimu nyingine ili kuziba pengo hilo kama ifuatavyo:

- (16) a. Kaa – Kalia (*Kaia)
b. Toa – Tolea (*Toea)

c. Noa – Nolea (*Noea)

Lugha ni mfumo unaoweza kubadilika kwa urahisi lakini wakati uo huo huwa na utaratibu wa kuhifadhi uadilifu na utaratibu wa kisarufi ili kuwawezesha wazungumzaji kuzungumza kwa ufanisi (Fasold & Connor-Linton, 2006). Misukosuko katika miundo ya lugha hupelekea lugha kubadilika. Uchopekaji wa aina hii hautokei kila mara na unahusishwa na lugha chache (Eshun, 2004). Uchopekaji huu ni sheria ya uziada katika Kiswahili. Sheria ya uziada ni sheria ibainikayo kwa sifa ya kutoathiri na kutoibua muundo mpya katika lugha. Sheria hii hutumika kufidia ujumbe ambao hauwezi kutabirika katika lugha. Mfanyiko huu wa uchopekaji hupelekea mabadiliko ya kimofolojia katika lugha yanayoweza kuelezwa kupitia kwa mfanyiko wa kifonolojia wa udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi.

HITIMISHO NA PENDEKEZO

Hitimisho: Aidha, katika kueleza changamoto zinazohusishwa na sababu za mabadiliko ya lugha, ilibainika kuwa ni vigumu kutenganisha vichocheo na sababu kamili za mabadiliko ya lugha. Pili, athari za mabadiliko ya lugha zinaweza kuingizwa kama maelezo ya sababu za mabadiliko ya lugha. Tatu, ilikuwa vigumu kubainisha mipaka baina ya sababu za kiisimu na kiisimu-jamii. Zaidi ya hayo, imebainika kuwa sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi haina tija katika Kiswahili cha sasa. Vilevile, makala hii ilionyesha kuwa mabadiliko mengine kama vile uchopekaji hutokea katika kiwango cha mofolojia ili kurekebisha makosa ya kimuundo katika lugha yanayosababishwa na badiliko la kwanza. Kando na haya, makala hii ilionyesha kuwa sheria ya udondoshaji wa kihistoria wa fonimu za likwidi haina tija katika Kiswahili cha sasa.

Pendekezo: Kuzuia uhomonimia na kuwepo kwa masalio ya kiisimu ni baadhi ya sababu zilizotolewa kueleza uzuiaji wa sheria.

REFERENCES.

- Aitchison, J. (1991). *Language Change: Progress or Decay* (3rd ed.) Cambridge University Press.
- Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. Macmillan Publishing CO., INC.
- BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Bostoen, K. & Bastin, Y. (2016). *Bantu Lexical Reconstructions*. Oxford Handbook Online: Online Publication. <https://doi.org/10.1093/oxfordhb/9780199935345.013.36>
- Campbell, L. (1999). *Historical Linguistics: An Introduction: The MIT Press*.
- Celce-Murcia, M., Brinton, D. M., Goodwin, J. M., & Griner, B. (2010). *Teaching Pronunciation: A course book and reference guide* (2nd ed.). Cambridge University Press.
- Crowley, T., & Bown, C. (2010). *An Introduction to Historical Linguistics*. (4thed). Oxford University Press.
- Eshun, F. (2004). Redundancy Rules in Kiswahili. *Occasional Papers in Language and Linguistics*, 2, 72-85. The University of Nairobi.
- Fasold, R. W., & Connor-Linton, J. (2006). *Introduction to Language and Linguistics*. (2nd ed.) Cambridge University Press.
- Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2002) *An Introduction to Language* (9th ed.) International edition Michael Rosenberg.
- Hayes, B. (2009). *Introductory Phonology*. Blackwell Publishing.
- Hinnebusch, T. J. (1973). *Prefixes, Sound Change and Subgrouping in the Coastal Kenyan Bantu Languages*. [Unpublished Ph.D Dissertation, Los Angeles: University of California].
- Kipacha, A. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kiplimo, C. E., & Mwita L. C. (2021). Thibitisho la Udondoshaji wa Kihistoria wa Fonimu za Likwidi. *East African Journal of Swahili Studies*, 4(1), 43-57. <https://doi.org/10.37284/eajss.4.1.474>.
- McGregor, W. B. (2009). *Linguistics: An Introduction*. Continuum International Publishing Group.
- Mgullu, S. R. (1999). *Mtaala wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziyyah*. Dar es Salaam: TUKI
- Nurse, D., & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. University of California Press.
- Postal, P. M. (1968). *Aspects of Phonological Theory*. Harper & Row.
- Schane, S. A. (1973). *Generative Phonology*. Prentice-Hall.
- Sommerstein, A. H. (1977). *Modern Phonology*. Edward Arnold.
- Trask, L. (2015). *Historical Linguistics*. (3rd ed). (R.M. Millar, Eds.). Routledge.